



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA
TEMEKE

07/02/2022

TAARIFA KWA UMMA
TAMKO LA UFAFANUZI

OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE INAPENDA KUTOA TAARIFA YA UFAFANUZI WA CHAPISHO LA HABARI LILILOTOLEWA TAREHE 05/02/2022 NA CHOMBO CHA HABARI CHA MTANDAONI KINACHOFAHAMIKA KAMA ANIMATTI MEDIA KUPITIA KURASA YAO YA INSTAGRAM KWA KUCHAPISHA TAARIFA YENYE KICHWA CHA HABARI "MADARASA YAGEUZWA KITUO CHA KUVUTA BANGI" SHULE YA MSINGI KIJICHI B(MTONI KIJICHI) ILIYOPO KATA YA KIJICHI WILAYA YA TEMEKE.

AIDHA OFISI YA MKURUGENZI INAFHAMU KUWA SHULE HIYO IMEKUWA IKIPITIA CHANGAMOTO YA WANAFUNZI WAKE KUCHANGIA UWANJA WA MICHEZO NA WANANCHI WALIPO JIRANI NA ENEO HILO KITU AMBACHO KIMEKUWA KIKISABABISHA UVUNJWAJI WA SHERIA KWA BAADHI YA WATU KUJIHUSISHA NA MATUMIZI YA MIHADARATI NA POMBE VINAVYOPELEKEA KULETA ATHARI KUBWA KWA WANAFUNZI WA SHULE HIYO.

KUTOKANA NA MUIINGILIANO HUO, BAADHI YA WATU WAOVU HUTUMIA FURSA HIYO KUTUMIA ENEO HILO LA UWANJA KAMA KIVULI CHA KUFANYIA MAOVU YAO NA KUJARIBU BAADHI YA MIUNDOBINU YA SHULE HIYO.

OFISI YA MKURUGENZI IMEJIRIDHISHA KUWA MATUMIZI YA MIHADARATI HIYO HUFANYWA KATIKA ENEO LA UWANJA NA SI KATIKA MADARASA YA SHULE HIYO KAMA ILIVYORIPOTIWA NA CHOMBO HICHO CHA HABARI.

OFISI YA MKURUGENZI INAPENDA KUUTARIFU UMMA KUWA TAARIFA YA CHANGAMOTO HII NA NYINGINE KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ZINAENDELEA KUSHUGHULIKIWA ILI KUHAKIKISHA USALAMA WA WANAFUNZI NA WALIMU UNAIMARISHWA KWENYE MAENEO HAYO.

TUNAPENDA KUWATOA HOFU WANANCHI WOTE WALIOPATA TAHARUKI KUTOKANA NA TAARIFA HIYO NA KUWAHAKIKISHIA KUWA UONGOZI WA MANISPAA UNA JUKUMU LA KULINDA USALAMA WA WANAFUNZI NA MIUNDOBINU YA SHULE ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE KUHAKIKISHA WANASOMA KWENYE MAZINGIRA RAFIKI NA SALAMA.

TAARIFA HII IMETOLEWA NA;


MKURUGENZI WA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

MKURUGENZI WA MANISPAA
TEMEKE